


# MUONGOZO WA UOMBAJI WA UFADHILI WA CHEVENING.



The screenshot shows the Chevening website header with the royal crest logo and navigation links: News & Blog, About us, Partner with us, Home, Search site. Below the header is a navigation bar with links: RESOURCE HUB, SCHOLARSHIPS, FELLOWSHIPS, OUR IMPACT, and a red APPLY button. The main banner features a group of eight diverse professionals standing outdoors. Overlaid on the banner is a white box with the text: **Chevening in Tanzania**, Study in the UK on a fully funded Chevening Scholarship, and a green dot icon followed by 'Open for applications until 5 November 2024, at 12:00 (GMT)'. Below the banner, a text line reads 'Applications for 2025-2026 Chevening Scholarships are now open!' with a red APPLY TODAY button. At the bottom, a small text block states: 'Chevening is the UK Government's international scholarships programme. Funded by the Foreign, Commonwealth and Development Office and partner organisations, we offer awards to study in the UK for one year on a fully funded master's degree course.'

Umetayarishwa na:

Mchaguliwa wa Ufadhili wa China (Selected candidate for CSC type A-Masters, 2024)

Mchaguliwa wa Ufadhili wa Commonwealth (Selected candidate for Commonwealth Masters Scholarships-2024)

TANBIHI:

Maoni yaliyotolewa katika muongozo huu yanatokana na uzoefu wa mwandishi na wala sio maoni ya Kamati ya ufadhili wa Chevening au Ofisi ya Maendeleo, mambo ya nje na Umoja wa madola (FCDO).

**Ruhusa ya kusambaza kwa kila anayehitaji imetolewa**

©2024

## YALIYOMO

KWA NINI NIMEANDIKA MUONGOZO HUU?.....	3
UTANGULIZI WA MWANDISHI. ....	4
MAELEZO JUU YA UFADHILI WA CHEVENING. ....	6
VIGEZO STAHIKI VYA UFADHILI HUU (ELIGIBILITY CRITERIA).....	7
NYARAKA ZINAZOHITAJIKA.....	8
HATUA ZA KUFANYA ILI KUOMBA UFADHILI HUU.....	8
JE NI LAZIMA UWE NA CHETI AU UFANYE MTHANI WA KIMATAIFA WA KIINGEREZA (IELTS AU TOEFL)? .....	9
NAMNA YA KUJIBU INSHA 4 ZA CHEVENING NA MIFANO.....	9
KUHUSU REFEREES.....	15
NAMNA YA KUOMBA VYUO VYA UINGEREZA. ....	16
KUHUSU DEPOSIT. ....	20
NAMNA YA KUANDIKA EMAIL .....	21
MIONGOZO MENGINE.....	21

## KWA NINI NIMEANDIKA MUONGOZO HUU?

Miongoni mwa yaliyonipelekea kuandaa muongozo huu ni pamoja na kuyaenzi maono ya viongozi waasisi wa Taifa na misingi ya SUZA (SUZA Core values) kama nilivyonukuu hapa chini:

NUKUU KUTOKA KWA VIONGOZI WAASISI WA TAIFA LA TANZANIA.



"Hakuna mtu anayetutaka kuwapenda wengine zaidi ya tunavyojipenda wenyewe, lakini kwa baadhi yetu tuliobahatika kupata elimu nzuri tunawajibika kuboresha ustawi wa jamii tunamoishi, ni sehemu ya kujipenda sisi wenyewe" Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere.



"Jambo moja ni wajibu wetu tukwambieni vijana. Jambo lenyewe ni hili, kwamba msidhani kuwa hii Serekali yenu itaendeshwa na watu wasiokuwa nyinyi. Ni heshima kubwa kila mwananchi leo aliye kijana, aliyesoma mpaka Darasa la nane au kuendelea mbele au asiyesoma nia iwe moja ya kujenga nchi..." Hayati Sheikh Abeid Amani Karume.



MIONGONI MWA NUKUU 3 KUTOKA KWENYE MISINGI MIKUU YA SUZA (SUZA Core Values)

- + Kupenda na kuchochea mabadiliko katika jamii (Embrace and drive changes)
- + Kuwa na mtazamo chanya kwa jamii (Good intentions)
- + Kuwa mzalendo kwa taifa. (Patriotism)

**Lengo kuu la kuandaa muongozo huu pamoja na miongozo mengine ya ufadhili, ni kuongeza uelewa kwa wataanzania wenzangu juu ya fursa hizi za ufadhili. Pia kuongeza idadi ya wataanzania wanaoomba na wanaochaguliwa katika fadhili hizi.**

**Pamoja na kuungana na juhudi za wataanzania wenzangu waliopata nafasi hizi na wanaowasaidia wengine kupata nafasi hizi.**

## UTANGULIZI WA MWANDISHI.

Ndugu watanzania wenzangu, tafadhali naomba mfahamu mambo kadhaa hasa katika kuomba ufadhili.

1. Kila ufadhili una vigezo vyake, hivyo unapaswa kujikita kwenye vigezo. Kuna baadhi ya ufadhili unaomba peke yake na chuo unaomba peke yake mfano Chevening, Commonwealth, Chinese Scholarship na kuna ufadhili unaomba na vyuo kwa pamoja katika ombi moja mfano Turkish Buslari scholarship, KNB Indonesian Scholarship na nyenginezo. Pia baadhi ya vigezo huwemo katika ufadhili Fulani na hukosekana kigezo hicho katika ufadhili fulani, mfano kigezo cha umri au uthibitisho wa ufasaha wa lugha ya kiingereza. Hivyo kabla ya kuanza maombi ya ufadhili au chuo husika, tafadhali pitia na soma maelekezo yote, hii itakusaidia kuwa na uhakika wa unachokifanya na kukuongezea nafasi ya kufanikiwa katika maombi yako.
2. Fadhili na vyuo vingi duniani vinavyopokea wanafunzi wa kimataifa (International students) huweka maelekezo juu ya namna ya kuomba, au huweka majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara (Frequently Asked Questions-FAQs) au huweka mawasiliano yao iwapo utahitaji kuwasiliana nao. Tafadhali hakikisha unasoma maelekezo haya au unapitia FAQs, na ikibidi fanya mawasiliano nao iwapo utakwama au utapata changamoto yoyote.
3. Tafadhali fahamu kuwa fadhili nyingi huwa na ushindani wa hali ya juu, hivyo hakikisha unakidhi vigezo husika lakini pia unafata maelekezo husika kabla hujaanza kufanya maombi husika. Kusoma maelekezo husika kutakusaidia kutambua nini unafanya na hii itakupunguzia maswali au sintofahamu inayojitokeza wakati unafanya maombi yako.
4. Kufanya maombi ya Fadhili hata kama ni za kulipiwa kila kitu (Fully funded) mara nyingi huhusisha gharama kama vile muda na pesa. Mfano unaweza kutumia pesa katika kutoa nakala, kuthibitisha nakala zako kwa mwanasheria, kubadilisha nyaraka ngumu kuwa nyaraka laini (scanning), kuperuzi mtandao na mambo mengine. Unapaswa kutenga masaa kadhaa kila siku kupitia taarifa za scholarship na kuangalia kama una sifa.
5. **JIAMINI**, kama wengine walipata ufadhili, hata na wewe unao uwezo wa kupata. Muhimu ni **KUJITUMA** na kufuata maelekezo yote yanayotakiwa. Tafadhali pitia mfano wa uandishi wa email ambao nimeuainisha katika muongozo huu ili utumie kama njia ya mawasiliano iwapo utahitaji kufanya hivyo. Kumbuka kuwa mawasiliano kwa njia ya email ndio njia kuu ya mawasiliano kwa fadhili au vyuo vya nje ya nchi.

6. Usisahau kumtanguliza Mwenyezi Mungu kwenye kila kitu ufanyacho. Kwa hakika haswa utakutana na changamoto kadhaa, tafadhali usikate tamaaa. Hata wengine pia walikutana na changamoto wakati wanaomba. Siku zote amini kuwa, aliyewawezesha wengine kupata ndiye atakayekuwezesha wewe kupata.
7. Jihadhari na **utapeli**, kwenye uombaji wa ufadhili kuna utapeli pia hivyo hakikisha unahakiki ufadhili/chuo husika ili kuepuka kutapeliwa. Kumbuka kuwa si kila tangazo la ufadhili/udahili ni la kweli.
8. Epuka kunakili taarifa za mitandaoni na badala yake andika maandiko yako au ikibidi kuchukua taarifa za mtandaoni basi mtaje na muandishi ili kuepuka kosa la kunakili (plagiarism). Kuwa mkweli katika maelezo yako wakati unaandaa Wasifu binafsi (CV) au mpango wa masomo (Study plan) au barua ya motisha (motivational letter) au insha (essays). Mara nyingi uitwapo katika usaili, baadhi ya maswali huulizwa kulingana na taarifa ulizojaza katika nyaraka nilizotaja hapo awali, sasa kama umedanganya itakuwa vigumu kwako kujitetea.
9. Unashauriwa kuomba fadhili nyingi kadiri uwezavyo kulingana na vigezo unavyokidhi. Hata hivyo, ushauri wangu ni kuchagua fadhili zisizopungua 3 na zisizozidi 10 na kuhakikisha unazifatilia kwa umakini mkubwa sana. Kumbuka kuwa, kuomba fadhili nyingi bila kufata maelekezo husika au kukidhi vigezo husika hakukuongezei nafasi ya kupata badala yake nafasi ya kupata inaongezeka iwapo utafata maelekezo/vigezo husika hata kama utaomba ufadhili mmoja tu. (Hoja sio wingi wa kuomba fadhili nyingi, bali kinachosisitizwa ni kufata maelekezo husika kisha kuomba fadhili husika)
10. Tafadhali tambua kuwa uombaji wa fadhili au vyuo unahitaji umakini wako. Usiharakishe kutuma maombi kabla hujasoma maelekezo husika. Mfano, kuna baadhi yetu walifika mpaka chuo husika walichoomba wakidhani kuwa fadhili waliyopata ni ya kulipiwa kila kitu (fully funded) hali yakuwa ni ya kulipiwa baadhi (partially funded) na hivyo kupelekea kusoma kwa shida, kupata msongo wa mawazo na athari nyengine. Yasingewapata haya laiti wangelisoma maelekezo husika ya fadhili/chuo kabla ya kuomba.
11. Nafahamu UGUMU unaopatikana wakati wa kufatilia fadhili mbalimbali lakini JITAHIIDI ufanye maombi wewe mwenyewe na sio kufanyiwa na mtu au wakala. Hii itakurahisishia wakati wa usaili (interview) kwa kuwa utakuwa unajuwa ulichokiandika wakati unafanya maombi.

**INDHARI:** Lengo la muongozo huu ni kukupa mwanga wa namna ya kuomba ufadhili au chuo husika. Mwandishi hatoi huduma ya kufanyia watu maombi ya ufadhili wa aina yeyote ile, lakini yupo tayari kukusaidia pale utakapokwama kwa fadhili ambazo ana uzowefu nazo. Aidha maoni yaliyoandikwa humu hayatokani na taasisi au bodi ya ufadhili husika bali yanatokana na uzoefu wa mwandishi katika ufadhili husika.

## MAELEZO JUU YA UFADHILI WA CHEVENING.

Huu ni ufadhili unaolipia kila kitu (fully funded scholarship) unaotolewa na Serekali ya Uingereza kupitia ofisi yake ya Mambo ya nje, Umoja wa madola na maendeleo, pamoja na vyuo vikuu vya Uingereza vilivyoingia makubaliano na program hii. Ufadhili huu ulianza rasmi mwaka 1983 na mpaka mwaka 2023, wanufaika 57,000 kutoka nchi mbalimbali wamenufaika na ufadhili huu.

Ufadhili huu ni miongoni mwa fadhili zenye ushindani mkubwa zaidi duniani. Mchakato wa ufadhili huu hutumia wastani wa miezi nane takriban, kuanzia siku ambayo dirisha la maombi linafungwa mpaka wanufaika wanawasili nchini Uingereza kwa ajili ya kuanza masomo. Kwa kawaida dirisha la maombi hufunguliwa mwezi wa August au Septemba na kufungwa Novemba kila mwaka.

Tambua kuwa dirisha la maombi likifunguliwa, maombi ambayo hupokelewa na kuchakatwa ni kwa ajili ya mwaka wa masomo unaoanza mwaka unaofata. Mfano, kwa mwaka huu 2024, dirisha limeshafunguliwa tangu tarehe 8 August hivyo iwapo utafanikiwa kupata ufadhili huu masomo yanatarajiwa kuanza Septemba/Octoba 2025. (yaani ukiomba mwaka huu maana yake unaomba kwa mwaka wa masomo 2025/2026 na sio 2024/2025)

Ufadhili huu unahusisha kwenda kusoma masomo ya shahada ya uzamili (Master's degree) nchini Uingereza kwa muda wa mwaka mmoja. Hii inamaanisha ufadhili huu hauhusishi shahada ya kwanza wala shahada ya umahiri (bachelor and PhD).

Baadhi ya faida za ufadhili huu ni pamoja na:

- ✚ Kusoma shahada ya uzamili ndani yam waka mmoja katika chuo kikuu cha Uingereza
- ✚ Kulipiwa ada ya masomo
- ✚ Kulipiwa Tiketi za ndege kwenda na kurudi nchini Uingereza.
- ✚ Kulipiwa gharama za Visa na bima ya afya
- ✚ Kulipiwa posho la kujikimu la kila mwezi uwapo Uingereza
- ✚ Kushiriki matukio mbalimbali yatakayosimamiwa na Chevening
- ✚ Kuungana na wanufaika wengine wa Chevening Zaidi ya 57,000
- ✚ Kujifunza tamaduni mpya ya watu wa Uingereza au watu wengine wanufaika wa Chevening



Mchakato wa ufadhili huu ni kama ifuatavyo:

Kufunguliwa kwa dirisha la maombi na kuanza kupokelewa kwa maombi ya ufadhili	Tarehe 8 August 10, 2024
Kufungwa kwa dirisha la maombi na mwisho wa kupokelewa kwa maombi ya ufadhili.	Tarehe 5 Novemba 2024
Maombi huangaliwa kama yamekidhi vigezo stahiki (eligibility criteria checkup)	Kuanzia Novemba 6 2024
Maombi kupitiwa na kamati ya kusoma maombi (Reading committee assessments)	Baina ya tarehe za kati za Novemba 2024 mpaka mwishoni mwa Januari 2025
Waombaji kuitwa katika usaili (interview)	Katikati ya Februari 2025
Mwisho wa kutuma nyaraka za kitaaluma (academic certificates) na mapendekezo (recomendations)	Tarehe 19 Februari 2025
Usaili unafanyika	Tarehe 26 Februari mpaka 25 April 2025
Matokeo ya ufadhili	Kuanzia Juni 2025
Tarehe ya mwisho ya kutuma barua ya udahili kutoka chuo cha Uingereza	Tarehe 11 Julai 2025
Kuanza kwa masomo nchini Uingereza	Septemba/Oktoba.

## VICEZO STAHIKI VYA UFADHILI HUU (ELIGIBILITY CRITERIA)

- Kuwa raia kutoka katika nchi zinazotambuliwa kama Chevening-eligible country, **Tanzania ni mojawapo.**
- Kujikubalisha kurudi nchini mwako baada ya kumaliza masomo ya shahada ya uzamili nchini Uingereza.
- Kuwa na uzoefu kazini usiopungua miaka miwili. Sio lazima uwe umeajiriwa, uzoefu huu wa kazini unahusisha uzoefu ulioupata katika kazi ulizojitolea, kazi ulizoajiriwa, kazi za mafunzo tarajali (internship), kazi ulizoajiriwa kwa muda, na kazi ulizoajiriwa za kudumu na zoefu nyengine mfano wake. Kwa bahati mbaya, mhitimu wa hivi karibuni 2024 na 2023 hatokishi kigezo hiki.
- Kuwa na shahada ya awali itakayokuwezesha kuweza kudahiliwa kwa ngazi ya shahada ya uzamili katika vyuo vya Uingereza.
- Ufanye maombi katika vyuo angalau vitatu vya Uingereza na uwe na barua japo moja ya udahili yenye masharti au isiyo na masharti (conditional or unconditional offer). Katika mfumo wa maombi ya ufadhili utaainisha na kutaja vyuo 3 pamoja na kada 3 unazotarajia kuomba huko Uingereza. Kumbuka kuwa hii barua ya udahili kutoka chuo cha Uingereza **sio lazima uipate** kabla ya tarehe ya mwisho (Novemba 5), unaruhusiwa kutuma maombi yako ya ufadhili bila ya barua ya udahili ya chuo. Barua hii itakua ni lazima uwe nayo kabla ya tarehe 11 Julai 2025 iwapo utafanikiwa kupata ufadhili huu, na ikiwa hutokuwa nayo basi hutoweza kuendelea na ufadhili huu. Hivyo, unashauriwa kufanya maombi ya chuo aidha sambamba na maombi ya ufadhili huu au punde tu baada ya kutuma maombi ya ufadhili.

## NYARAKA ZINAZOHITAJIKA.

- ✚ Nyaraka za kitaaluma (Academic certificates and transcripts)
- ✚ Wadhamini wawili wa kitaaluma (Two academic referees)
- ✚ Barua ya udahili kutoka chuo cha Uingereza-hii kwa tarehe za mbeleni. (unaweza kutuma maombi ya ufadhili bila barua hii)
- ✚ Hati/pasi ya kusafiria

## HATUA ZA KUFANYA ILI KUOMBA UFADHILI HUU.

- ✚ Hatua ya kwanza: Angalia kama unakidhi vigezo (tafadhali tembelea kiunganishi hiki <https://www.chevening.org/resource-hub/guidance/eligibility/>)
- ✚ Hatua ya pili: Chagua kada 3 za shahada ya uzamili katika vyuo vya Uingereza. (tafadhali tembelea kiunganishi hiki <https://www.chevening.org/scholarships/find-a-course/>) kumbuka kuanza kufanya maombi katika kada ulizoainisha mara tu baada ya kumaliza maombi ya Chevening.
- ✚ Hatua ya tatu: Andaa nyaraka zako za kitaaluma na taarifa zako za wadhamini. (tafadhali tembelea kiunganishi hiki <https://www.chevening.org/resource-hub/guidance/references/>) kumbuka kuwa nyaraka laini ya vyeti vyako halisi sio nakala ndio vinavyohitajika hapa (yaani scan vyeti na transcript halisi na sio nakala pia huhitaji kuvipiga muhuri wa mwanasheria kwa kuwa umescan nyeti halisi na sio nakala). Pia utawasilisha taarifa na mawasiliano ya wadhamini wako wakati unafanya maombi, baada ya kuitwa kwenye usajili ndio utalazimika kuzituma/kwenda na nyaraka.
- ✚ Hatua ya nne: Kamilisha maombi yako na utume. Hapa utapaswa kujibu insha 4 (essays) kwa uchache wa maneno 100 na ukomo wa maneno 500 kwa kila moja ambazo zinahusu:
  1. Leadership and influence
  2. Relationship-building and shared learning
  3. Studying in the UK and
  4. Your long-term career goals.

Insha hizi ndio moyo wa maombi yako, hivyo jitahidi kufanya vizuri wakati unajibu insha hizi. Nitaelezea namna ya ujibuji wake huko mbeleni.

Tafadhali tembelea viunganishi hivi kujua zaidi juu ya ushauri kwa waombaji <https://www.chevening.org/news/application-advice/>  
<https://www.chevening.org/news/what-leadership-qualities-do-you-need-to-become-a-chevening-scholar/>

Tafadhali tembelea kiunganishi hiki kujua zaidi juu ya namna ya kutumia mfumo wa maombi ya ufadhili huu, <https://www.chevening.org/resource-hub/guidance/online-application-system/>)



Ili kuanza kufanya maombi katika mfumo tafadhali tembelea kiunganishi hiki <https://asams.chevening.org/apply>

Usisahau kupitia ukurasa wa majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara kupitia kiunganishi hiki <https://www.chevening.org/FAQs>

Pia usisahau kupitia kiunganishi hiki ili kujua makosa yanayorudiwa na waombaji ili uweze kuyaepuka <https://www.chevening.org/resource-hub/guidance/common-errors/>

- ✚ Hatua ya tano: Baada ya kutuma maombi yako, subiri usaili. Iwapo utafanikiwa kuitwa katika usajili tafadhali tembelea kinganishi hiki ili kujiandaa <https://www.chevening.org/resource-hub/guidance/interviews/>
- ✚ Hatua ya sita: Fanya maombi katika zile kada 3 ulizochagua katika vyuo vya Uingereza na hakikisha unapata barua ya udahili isiyo na masharti (unconditional offer) kabla ya Julai 11 2025. Tafadhali tembelea kinganishi hiki <https://www.chevening.org/resource-hub/guidance/university-applications/>
- ✚ Nitaelezea namna ya kufanya maombi katika vyuo vya Uingereza huko mbeleni.
- ✚ Hatua ya saba: Iwapo utafanikiwa katika hatua ya usaili kisha hatua ya kupata ufadhili huu, hongera juu yako. Usisahau kuwasaidia wataanzania wengine na wao waweze kufanikiwa kama ulivyofanikiwa wewe.

## JE NI LAZIMA UWE NA CHETI AU UFANYE MTHANI WA KIMATAIFA WA KIINGEREZA (IELTS AU TOEFL)?

Jambo jema ni kuwa Ufadhili huu wa Chevening hauna kigezo cha ulazima wa kuwa na cheti cha kuthibitisha ufasaha wa lugha ya kiingereza. Hata hivyo, uandishi wako wa insha utatumika kukupima uwezo wako katika kuandika na kufikisha ujumbe kwa kiingereza. Pia wakati wa usaili (interview) uwezo wako wa kuzungumza kiingereza utapimwa.

Aidha vyuo vingi vya Uingereza vinahitaji vyeti hivi vya ufasaha hasa IELTS. Nikutoe wasiwasi kuwa unaweza kupata udahili kutoka katika vyuo vya Uingereza bila ya kuwa na vyeti hivi (Nitaelezea huko mbeleni).

Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kuwa iwapo utafanikiwa kupata ufadhili huu masomo pamoja na mazingira yako yatakuwa ni kwa lugha ya kiingereza kwa asilimia 100. Ni juu yako kuhakikisha unajua lugha hii kwa ufasaha ili kuepuka madhara kama kufeli na msongo wa mawazo.

## NAMNA YA KUJIBU INSHA 4 ZA CHEVENING NA MIFANO

Ikumbukwe kuwa mimi sijaomba ufadhili huu, hivyo maelezo niliyoyatanguliza na ninayoendelea kuyatoa kuhusu ufadhili huu ni kutokana na uzoefu niliopata wakati naomba ufadhili wa Commonwealth Masters Scholarship ambao ndio nilioupata. Fadhili hizi (yaani Chevening na Commonwealth zinafanana sana (zote zinatolewa na Serekali ya Uingereza kupitia ofisi ya maendeleo, mambo ya nje na Umoja wa Madola) isipokuwa tofauti ni ndogo sana).

Pia nilihudhuria kongamano lililofanyika kupitia mtandao wa youtube lilifanywa na balozi ya Tanzania nchini Uingereza inayoongozwa na Mhe. Mbelwa Kairuki mwezi March 2024. Pia nilipata nafasi kuhudhuria kongamano la Zanzibar Scholarship Fair lililofanyika mwezi wa April katika hotel ya Zanzibar Beach Resort. Makongamano yote haya yalihudhuriwa na wajumbe kutoka Balozi ya Uingereza nchini Tanzania ambao walielezea kwa kina kuhusu ufadhili huu wa Chevening.


Kama nilivyotangulia kusema hapo awali kuwa insha hizi ndio moyo wa maombi yako katika ufadhili huu. Ukiharibu katika insha ndio umeshaharibu maombi yako. Tafadhali tumia muda mwingi kuandaa insha hizi. Una takriban siku 80 za kuandaa insha hizi kabla ya kufungwa kwa dirisha la maombi ya ufadhili huu. Tafadhali tembelea viunganishi vifuatavyo ili uweze kujifunza vizuri namna bora ya kujibu insha hizi. Tafadhali chukua kalamu na daftari uwe unaandika vitu muhimu wakati unapitia viunganishi hivi. Ni matumaini yangu kuwa iwapo utapitia viunganishi hivi, utafanikiwa kupata ufadhili huu (Usisahau kutumia mitandao kama Grammarly ili kurekebisha makosa ya kiuandishi wakati unaandika insha zako).

Tafadhali tembelea kiunganishi hiki ili kujifunza zaidi juu ya Chevening kutoka kwa mnufaika wa ufadhili huu. [https://youtube.com/playlist?list=PLHZYXfQI6b8M3ZGV-W5a\\_KBr1-nG9n3z&feature=shared](https://youtube.com/playlist?list=PLHZYXfQI6b8M3ZGV-W5a_KBr1-nG9n3z&feature=shared)

Baada ya kuandaa Insha zako, sasa unaweza kuanza maombi. Tafadhali tembelea kiunganishi hiki:

<https://asams.chevening.org/apply>

Chagua nchi (Tanzania), kisha chagua Chevening scholarship 2025/2026. Kisha Endelea



The screenshot shows the Chevening application website. The header is black with the word 'Chevening' in white. Below the header, the main heading is 'Choose an award'. Under this heading, there are two sections: 'Choose the country or territory you are applying for' with a dropdown menu showing 'Tanzania', and 'Choose the award you are applying for' with a radio button selected for 'Chevening Scholarship 2025-2026'. Below the radio button, there is a description: 'We provide fully funded scholarships for one-year master's degrees. Outpace your peers and return home with the skills, knowledge and network required to influence positive change.' At the bottom of the form is a green 'Continue' button. The footer of the website is light grey and contains the logo of the Foreign, Commonwealth & Development Office on the left and the Chevening logo on the right.

Utafunguka ukurasa wa kujisajili, jaza email, namba ya sim una email mbadala.

ASAMS x +

asams.chevening.org/apply/email

**Chevening**

### Register for an account

Before you continue, please read the [Chevening Scholarship Terms and Conditions](#).  
[How the British Council manages personal data](#).

**Email address**  
Please use a personal email address and not an email address provided by an employer.

**Mobile number**  
Select the country calling code and then enter the phone number (digits only). If you lose access to your application, this may be used for recovery.

**Recovery email address**  
Please use a personal email address and not an email address provided by an employer. If you lose access to your application, this email address may be used for recovery.

☒ I agree that I have read and understood the [Chevening Scholarship Terms and Conditions](#), [Privacy Notice](#), and consent to the [British Council processing my personal data](#).

Utatumiwa kiunganishi katika hiyo email uliyoiandika hapo juu. Bonyeza kiunganishi hicho na utakutana na Eligibility page.

ASAMS x +

asams.chevening.org/application/eligibility

**Chevening**

### Eligibility requirements (Page 1 of 2)

Are you a citizen of a Chevening-eligible country / territory?

☐ Yes ☐ No

Will you return to the country of nationality/territory of which you are applying for a Chevening award after your studies have ended?

☐ Yes ☐ No

I understand that Chevening opportunities for study in the UK are not an exception to the return home policy and agree to not apply for any other visa category in the UK?

☐ Yes ☐ No

Do you have, or will you currently be working for, a recognised undergraduate degree that will be needed for entry onto a Chevening programme in the UK (minimum)?

☐ Yes ☐ No

Will you normally be required to obtain other qualifications (e.g. 11) before a degree is issued?

☐ Yes ☐ No

Do you hold at least 2 years' work experience?

☐ Yes ☐ No

Do you have completed your undergraduate degree before the date of submitting this application?

☐ Yes ☐ No

Are you applying for a scholarship for a course of study commencing in the UK between June 2021?

☐ Yes ☐ No

Foreign, Commonwealth & Development Office

[How we support](#) [Visas](#) [Fees](#) [Successful candidates](#) [Terms and conditions](#)

©CCL All content is available under the [Open Government Licence v3.0](#), except where otherwise stated

Tafadhali jibu maswali hayo kwa umakini kwa kuwa iwapo utakosea, ndio utakuwa umekosa vigezo vya kuendelea. Ukiyajibu kwa usahihi utatumiwa kiunganishi katika email yako.

## You have passed the eligibility check

You will receive further instructions in your email, to continue with your application. Please check your inbox, junk and spam folders.

Ukifungua kiunganishi utaletewa Access code. **Tafadhali itunze code hii kwa kuwa hutoweza kuendelea na maombi haya iwapo utapoteza code hii.**

### Make a note of your access code

You have passed the initial eligibility check for Chevening Scholarship 2025-2026.

Be sure to take a photo of your code or write it down in a secure place. You will need this code every time you access your application, and you will not be able to complete your application without it. **You will not be shown this access code again.**

You will not receive this code by email. If your code is lost, you may have to restart your application.

Your access code is:

1st	2nd	3rd	4th	5th	6th	7th	8th
Q	C	V	R	R	C	L	C

[Copy access code to clipboard](#)

[Continue](#)

**Access code** ndio utakayotumia kuendelea na maombi yako. Sio lazima umalize maombi haya kwa siku moja au kwa mda mmoja. Unaruhusiwa kujiandaa kidogkidogo. Itakupasa utumie kiunganishi cha mwisho ulichotumiwa na Chevening chenye ujumbe "Keep this email...."

ASAMS x ASAMS x +

asams.chevening.org/application/access-code-setup

## Chevening

### You can now continue with your application


**Next steps**

You will receive an email with a link to access your application. Please check your inbox, junk and spam folders.


When you click on the link, you will be prompted to confirm your identity by providing your 8 character access code, before you can access your application.

Please save this most recent email to access the application portal in future.

[Continue application](#)



Foreign, Commonwealth & Development Office



CHEVENING

[About and support](#) [Privacy](#) [Cookies](#) [Accessibility statement](#) [Terms and conditions](#)

**OGL** All content is available under the [Open Government Licence v3.0](#), except where otherwise stated

## Kuwa makini wakati wa ujazaji wa Access code

ASAMS x +

asams.chevening.org/application/validate-access-code

## Chevening


### Enter your access code

Enter the 2nd, 3rd, and 6th characters of your access code


1st	2nd	3rd	4th	5th	6th	7th	8th
	C	V			q		

[Continue to application](#)

[Recover your code](#) if you do not have your access code.



Foreign, Commonwealth & Development Office



CHEVENING

[About and support](#) [Privacy](#) [Cookies](#) [Accessibility statement](#) [Terms and conditions](#)

**OGL** All content is available under the [Open Government Licence v3.0](#), except where otherwise stated

Anza kujaza kila sehemu inayohitajika kwa umakini mkubwa. Tafadhali usifanye haraka ukaharibu, una siku Zaidi ya 80 takriban za kuyafanya bora maombi yako

ASAMS

asams.chevening.org/application/tasks

**Chevening** Apply for another award Sign out

**Important**

The deadline for submitting this application is 11:59 UTC on 5 November 2024.

## Application for Chevening Scholarship 2025-2026

Your application has not been submitted

### Make application

You have until 11:59 UTC on 5 November 2024 to submit your application, once submitted you will no longer be able to make amendments.

<a href="#">Personal details</a>	NOT STARTED
<a href="#">Citizenship and travel documents</a>	NOT STARTED
<a href="#">Higher education history</a>	NOT STARTED
<a href="#">Work history</a>	NOT STARTED
<a href="#">Programme of study</a>	NOT STARTED
<a href="#">Referees</a>	NOT STARTED

Sehemu ya Supporting statements ndio ambapo utaandika insha zako. Unashauriwa kuziandaa pembeni kisha uje uzikopie hapa katika mfumo ziwapo tayari (usiziandikie hapa katika mfumo)

ASAMS

asams.chevening.org/application/essays

**Chevening** Apply for another award Sign out

[Task list](#) > Supporting statements

## Supporting statements

All answers must be written in English. Applicants must not repeat answers. Use examples to support your answers.

### 1. Leadership and influence

Chevening is looking for individuals who will be future leaders or influencers in their home countries. Explain how you meet this requirement, using clear examples of your own leadership and influencing skills to support your answer.

You must enter a minimum of 100 words and a maximum of 500 words. (0 words entered)

### 2. Relationship building and shared learning

Chevening is looking for individuals with strong professional relationship-building skills, who will engage with the Chevening community and influence and lead others in their chosen profession. Please explain how you build and maintain relationships in a professional capacity, using clear examples of how you currently do this, and outline how you hope to use these skills in the future.

Usisahau kubonyeza "save progress" kila mara ili mfumo uhifadhi majibu yako.



ASAMS

asams.chevening.org/application/essays

### 3. Studying in the UK

Outline why you have selected your chosen three university courses, and explain how this relates to your previous academic or professional experience and your plans for the future. Please enter new information and examples here and not duplicate the information you have entered on the work experience and education section of this form.

You must enter a minimum of 100 words and a maximum of 500 words. (0 words entered)

### 4. Career plan

Chevening is looking for individuals who have a clear post-study career plan. Please outline your immediate plans upon returning home and your longer term career goals. You may wish to consider how these relate to what the UK government is doing in your country.

You must enter a minimum of 100 words and a maximum of 500 words. (0 words entered)

[Save progress](#) [Save and complete](#)

[Return to overview](#) (your data will not be saved)

Sehemu ya "Proposed Program of study" utachagua kada 3 kama maelekezo yanavoeleza. Kada hizo ni aidha zenye kufanana katika vyuo 3 tofauti au kada 3 zenye kutofautiana katika chuo kimoja au kada 3 zenye kutofautiana katika vyuo 3. Chagua NO kwenye swali "Have you already applied to this course?" ikiwa hujaanza kuomba chuo chochote. KUMBUKA kuanza kuomba kada ulizoainisha katika vyuo husika punde tu baada ya kukamilisha maombi katika mfumo huu.

ASAMS

asams.chevening.org/application/proposed-courses

Chevening [Apply for another award](#) [Sign out](#)

[Back](#) > [Proposed programme of study](#) > Add proposed programme of study

### Add a proposed programme of study

Institution name

Title of course / research

Select an institution

Course or degree type

Have you already applied to this course?

☐ Yes - I have a conditional offer

☐ Yes - I have an unconditional offer

☐ No

☐ Yes - rejected

☐ Yes - I'm awaiting a decision

[Save and close](#)

[Close](#)

Foreign, Commonwealth & Development Office

[About and support](#) [Privacy](#) [Cookies](#) [Accessibility statement](#) [Terms and conditions](#)

CC BY All content is available under the [Open Government Licence v3.0](#), except where otherwise stated

Tafadhali malizia sehemu zote kwa usahihi kisha kamilisha maombi yako.

## KUHUSU REFEREES.

Tafadhali ongea na referees wako mapema na wajulishe kuwa unatarajia kuomba Chevening na vyuo pia. Pia wajulishe kuwa kuna muongozo juu ya uandishi wa

reference/recommendation letter za Chevening katika kiunganishi hiki <https://www.chevening.org/resource-hub/guidance/references/>

## NAMNA YA KUOMBA VYUO VYA UINGEREZA.

Kuchagua kada bonyeza kiunganishi hiki <https://www.chevening.org/scholarships/find-a-course/>

Selecting the right courses at the right universities is one of the most important aspects of your application. Use this course finder tool to search for eligible master's degree programmes at every university across the UK\*.

Your Chevening application must list three courses, and they must be courses that are eligible for a Chevening Scholarship.

You will need to apply separately for your course via the university that runs the course. Your Chevening application does not constitute an application to your chosen courses.

\*The course information displayed in the finder is supplied by Postgrad Solutions. This data is regularly updated but, due to evolving course offerings at universities, it may not always be 100% accurate at the time of search. Candidates are responsible for checking that the courses they list in their application meet the criteria for Chevening funding. The Secretariat completes final checks on courses that candidates have selected following the interview period, and any courses that do not meet the criteria will be deemed ineligible. Please also check individual university websites for more information.

*In this section*

- Why study in the UK?
- Who can apply?
- Application timeline
- Find a course**
- FAQs

Powered by: **POSTGRAD**.com

Mimi nimetafuta kwa kuandika "Agricultural economics" na matokeo yakaja hivi:

university websites for more information.

Search results for 'Agricultural economics' in 'All regions'.

**Postgraduate Courses in Agricultural Economics**

1 PAGE 1 OF 1

✓ **CHEVENING PARTNER**

**UNIVERSITY OF READING**  
GRADUATE INSTITUTE OF INTERNATIONAL DEVELOPMENT AND APPLIED ECONOMICS

**Agricultural Economics**  
MSc

University of Reading

1 PAGE 1 OF 1

Bonyeza kada husika ili upate maelezo ya kada hiyo, chuo, mahitaji ya kada na mengineyo, mfano kama hivi:

ASAMS x Preparing your UK university ap x Find a course | Chevening x +

chevening.org/scholarships/find-a-course/

SEARCH AGAIN BACK TO SEARCH RESULTS

## University of Reading: Agricultural Economics

Institution	University of Reading
Department	Graduate Institute of International Development and Applied Economics
Web	<a href="https://www.reading.ac.uk">https://www.reading.ac.uk</a>
Email	<a href="mailto:pgadmissions@reading.ac.uk">pgadmissions@reading.ac.uk</a>
Telephone	0118 378 5289
Study type	Taught

MSc

Full-Time, 12 months starts Sep 2024

### Summary

Develop your understanding of economic concepts and policies that promote world agricultural development with our MSc Agriculture Economics master's degree.

With an ever-increasing world population and growing pressure on the world's finite resources, the analytical skills of agricultural economists are more relevant than ever.

\*\*For more information, please visit the programme page: <https://www.reading.ac.uk/ready-to-study/study/subject-area/international-development-and-applied-economics-pg/msc-agricultural-economics>\*\*

Level	RQF Level 7
Entry requirements	IELTS: 6.5 overall with no element less than 5.5 (or equivalent)

Applicants are normally required to have a good undergraduate honours degree, ideally with upper second-class or above (or equivalent from an internationally recognised university outside the UK), plus an intermediate knowledge of

Angalia "Entry requirements" ili ujue kama unakidhi kuomba. Sehemu niliyoikozesha kwa rangi ya bluu inanihitaji niwe na IELTS score ya 6.5, kama unavoona:

ASAMS x Preparing your UK university ap x Find a course | Chevening x +

chevening.org/scholarships/find-a-course/

Full-Time, 12 months starts Sep 2024

### Summary

Develop your understanding of economic concepts and policies that promote world agricultural development with our MSc Agriculture Economics master's degree.

With an ever-increasing world population and growing pressure on the world's finite resources, the analytical skills of agricultural economists are more relevant than ever.

\*\*For more information, please visit the programme page: <https://www.reading.ac.uk/ready-to-study/study/subject-area/international-development-and-applied-economics-pg/msc-agricultural-economics>\*\*

Level	RQF Level 7
Entry requirements	IELTS: 6.5 overall with no element less than 5.5 (or equivalent)

Applicants are normally required to have a good undergraduate honours degree, ideally with upper second-class or above (or equivalent from an internationally recognised university outside the UK), plus an intermediate knowledge of microeconomics and quantitative methods. Applicants who have relevant career experience are also welcome to apply.

Students may join immediately after their undergraduate degree, or after some years of employment to enhance career prospects by acquiring further skills.

Please note: if you have little or no training in economics, you may be admitted if you attend our pre-sessional economics course.

Location	University of Reading Whiteknights House PO Box 217 Reading RG6 6UR
----------	---


Full-Time, 12 months started Sep 2023

### Summary

Lakini mimi sina. **USIHOFU** ingia katika tovuti ya chuo husika kisha fanya maombi kama kawaida. Mfano, mimi niliingia tovuti ya **University of Reading** na nikafanya maombi ya kada ya "MSc Agricultural Economics". Sehemu ya IELTS niliweka barua ya uthibitisho wa kusoma shahada ya awali kwa kiingereza niliyopewa na chuo.



Chuo kilinijibu maombi yangu kama ifuatavyo:



Mahali pa kuzingatia ni hapa:



for the MSc in Agricultural Economics (full time)

**Your offer is conditional upon satisfying the following conditions** by the Programme Start Date:

Achieve a minimum score of 6.5 in IELTS (Academic) (with no element scoring below 5.5) or the equivalent score in one of our other acceptable English qualifications. A list of ones we accept with scores is available at [www.rdg.ac.uk/ad-EnglishTests.aspx](http://www.rdg.ac.uk/ad-EnglishTests.aspx)

Submit two satisfactory references. Please ensure that your references are sent directly from your referees professional or institutional email account.

Please note that we cannot accept the document you have provided as confirmation of your English language proficiency. A list of acceptable proficiency tests is available at [www.rdg.ac.uk/ad-EnglishTests.aspx](http://www.rdg.ac.uk/ad-EnglishTests.aspx)

Attached to this letter you will find the **Terms and Conditions for**

Kwamba wamenipa offer kusoma MSc Agricultural Economics lakini kwa sharti kuwa niwapelekee IELTS na recommendation 2 kutoka kwa referees wawili. Kumbuka hio statement "Please note that we cannot accept the document you have provided as confirmation of your English language proficiency" inaikataa ile barua niliyopewa chuoni kama nilivyoiweka hapo juu.

Lakini wametuma kiunganishi hapo kinachosema "A list of ones we accept with scores is available at [www.rdg.ac.uk/ad-EnglishTests.aspx](http://www.rdg.ac.uk/ad-EnglishTests.aspx)" Ukifungua kiungo hiki utagundua kuwa grade B ya English language katika cheti cha O level kinapokelewa na chuo hiki (na vyuo vyengine) kama kithibitisho kuwa unaweza kumudu kuwasilianana kwa kiingereza. Angalia picha hapo chini, na hivi ndivyo nilivyoweza kupata "unconditional offer" kutoka University of Reading.

**ZINGATIA:** Inakuhitaji kuchangamka, kuwa makini na kusoma kila unachoelekezwa, laiti nisingelisoma maelekezo husika nisingeweza kubaini jambo hili. Tafadhali uliza au fanya mawasiliano na wahusika kama timu ya udahili (admission team) iwapo utapata chanagmoto yoyote. Muhimu ni kujua namna ya kuwasiliana hasa kwa kutumia email.

Acceptable English Language p x +

reading.ac.uk/admissions/acceptable-english-language-proficiency-tests

University of Reading Admissions Staff Student A-Z lists

Information for staff

Admissions policies and procedures

Acceptable English language tests

Contact us

## Acceptable English Language tests

This page contains a guide to the only acceptable English language tests that can be used to meet a condition of offer (normally made in terms of IELTS scores) made by the University of Reading.

If the test you are intending to take is not listed, please contact the Admissions Team for advice using the details on the right.

Please note that this information may change as rules on acceptability change so please do keep checking back.

### Tests acceptable for entry onto a Pre-sessional English programme

Test	Test name
Cambridge	IELTS (Academic) for UKVI SELT
Cambridge	IELTS Online
CBSE/ICSE/ State boards	Indian Standard XII English (English Core/ English Elective/ Functional English)
CSE	National Examinations Council of Tanzania Certificate of Secondary Education (or Secondary Leaving Certificate)
Duolingo	Duolingo English Note: Not acceptable for Speech & Language Therapy programmes
ETS	TOEFL: Internet (our DI code is 0769)
ETS	TOEFL at home iBT

**Contact Admissions**

**International Foundation Programme**  
ifpadmissions@reading.ac.uk

**Undergraduate Programmes (full- and part-time)**  
ugadmissions@reading.ac.uk

**Postgraduate (taught and research) Programmes**  
pgadmissions@reading.ac.uk

**PGCE Programmes**  
teachertraining@reading.ac.uk

Acceptable English Language p x +

reading.ac.uk/admissions/acceptable-english-language-proficiency-tests

Cambridge	IELTS (Academic) for UKVI SELT
Cambridge	IELTS Online
CBSE/ICSE/ State boards	Indian Standard XII English (English Core/ English Elective/ Functional English)
CSE	National Examinations Council of Tanzania Certificate of Secondary Education (or Secondary Leaving Certificate)
Duolingo	Duolingo English Note: Not acceptable for Speech & Language Therapy programmes
ETS	TOEFL: Internet (our DI code is 0769)
ETS	TOEFL at home iBT


## KUHUSU DEPOSIT.

Vyuo vingi baada ya kukupa offer (aidha conditional au unconditional) watakwambia kuwa unahitajika kulipa "DEPOSIT" ili kuwahakikishia kuwa offer yako utaikubali. Mara nyingi huwa ni paund 2,000 (takriban mil6.5 za kitanzania) kwa vyuo vingi (japo hutofautiana). Hutakiwi kulipa hii, unachotakiwa kufanya ni kuwapa taarifa kuwa upo katika mchakato wa kuomba Chevening scholarship hivyo wasubiri mpaka majibu ya ufadhili yakitoka.



## NAMNA YA KUANDIKA EMAIL

Andika kichwa cha habari (heading) katika "Subject" na maelezo yako katika "Compose", Anza na salamu, jitambulisha kisha elezea hitajio lako, mfano:



## MIONGOZO MENGINE

Usikose Kufatilia Miongozo Mengine Kama Vile:

Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Commonwealth Masters and PhD

Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Serekali ya China (CSC type A &B)

Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Serekali ya Indonesia (KNB)

Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa India (ICCR)

Na miongozo mengine kadri nitakavyoweza kuiandaa kulingana na uzoefu niliopata wakati naomba fadhili mbalimbali (Fadhili zote tajwa hapo juu niliziomba isipokuwa ICCR). Tafadhali tumia kiunganishi hiki ([https://drive.google.com/drive/folders/1TfyG9g-YRh1K77ODKIZqd1dNeVXQYBsM?usp=drive link](https://drive.google.com/drive/folders/1TfyG9g-YRh1K77ODKIZqd1dNeVXQYBsM?usp=drive_link)) ili kuweza kuangalia miongozo mengine ya fadhili mbalimbali pindi iwapo tayari.

*MPAKA KUFIKIA HAPA SINA ZAIDI YA KUKUTAKIA KILA LA KHERI NA MAFANIKIO MEMA.  
NATUMAI MUONGOZO HUU UTAKUFAA NA UTAWAFAA WENGINE.  
AHSANTE.*

**Ruhusa ya kusambaza kwa kila anayehitaji imetolewa**

©2024

Iwapo utakuwa na maswali na utahitaji msaada tafadhali wasiliana nami kupitia:

[mahfoudh.mahfoudh@suza.ac.tz](mailto:mahfoudh.mahfoudh@suza.ac.tz) au 0787483930 (Whatsap only)

Au jiunge na kundi sogozi la Whatssap la "Scholarship for Tanzanians" kupitia kiuongo hiki:

<https://chat.whatsapp.com/F1L7kVdNALO7NTcUUZbnXP>

Kwa msaada mahsusi kuhusu Chevening Scholarship jiunge na kundi la "25/26 Chevening Aspirants" kupitia kiuongo hiki: <https://chat.whatsapp.com/LADiHgCRXh1IrykbkruAvc>

Ni mimi ninayejali mafanikio yako:

Mahfoudh Mohamed Mahfoudh

Msimamizi wa semina (Tutorial Assistant-Agribusiness)

Department of Agricultural Extension and Community Development

School of Agriculture

State University of Zanzibar.